

## **ACTIVE VOICE (KAULI YA KUTENDA)**

Katika ACTIVE VOICE (kauli ya kutenda) tenses huonesha mtendaji wa jambo

### **1. PRESENT TENSE (wakati uliopo)**

Present tense huonyesha tendo linalofanyika mara kwa mara

#### **First Formular = kanuni ya kwanza**

Pronoun + infinitive ya verb

Angalizo: katika nafsi ya tatu umoja yaani he/she/it ongeza s katika infinitive ispokuwa kwa vitenzi vinavyoishia na o, h, x na y inayotanguliwa na consonant ambazo ni alphabet zote ukiacha "a e i o u" kwa vitenzi vinavyoishia na y ianayotanguliwa na consonant(b, c, d, f, g, h, j...) toa y ongeza ies mfano: Cry = Cries kwa vitenzi vinavyoishia na o, h, na x ongeza es mfano:

Go = goes, Brush = Brushes, fix = fixes

## **singular**

1st person: I go (huwa naenda)

2nd person: You go (huwa unaenda)

3rd person: He/she/it goes (huwa anaenda)

## **plural**

1st person: We go (huwa tunaenda)

2nd person: You go (huwa mnaenda)

3rd person: They go (huwa wanaenda)

## **Mfano:**

She cleans = huwa anasafisha.

She mixes = huwa anachanganya.

## **Second formular**

Hutumika katika kukanusha yaani negation na

katika kuuliza maswali yaani asking

questions

Pronoun+ do+ infinitive ya verbs

## **singular**

1st person: I do go (huwa naenda)

2nd person: You do go (huwa unaenda)

3rd person: He does go (huwa anaenda)

## **plural**

1st person: We do go (huwa tunaenda)

2nd person: You do go (huwa mnaenda)

3rd person: They do go (huwa wanaenda).

## **NEGATIVE FORM/NEGATION**

### **(kukanusha);**

weka **'NOT'** baada ya **do** upate **do not**  
ambayo inaweza kufupishwa na kuwa  
kuwa **don't**

### **Mfano;**

- I do not want this/ I don't want this=sihitaji hiki
- He does not come here often/ he doesn't come here often= haji hapa mara kwa mara

## **MAKING QUESTIONS**

### **(namna ya kuuliza maswali);**

ianze sentensi na **do** au **don't** kama ni ya kukanusha, **mfano;**

Do you know?=unajua?

Does she study?=anasoma?

Don't they come?=hawaji?